TANGAZO LA SERIKALI NA. 544 la tarehe 5/7/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA RONDO YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Rondo ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Rondo.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA LINDI

MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA RONDO

Makadirio ya Eneo: Hekta 11742.28 au Kilometa za Mraba 117.42

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Rondo linalopatikana Wilaya ya Lindi, Mkoa wa Lindi kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2864 ya mwaka 2013 (Skeli 1:25,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo La Serikali Na. 544 (Linaendelea)*




Dodoma, <br>
___24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI <br>
*Waziri wa Maliasili na Utalii*